JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UCHUKUZI

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

TAARIFA YA HALI MBAYA YA HEWA KWA MWEZI SEPTEMBA NA OKTOBA, 2026

1.0 UTANGULIZI

Katika kipindi cha mwezi Septemba 2026, hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi, ikiambatana na hali ya baridi ya wastani, hususani nyakati za usiku na alfajiri katika maeneo machache ya nyanda za juu kusini magharibi. Mwanzoni mwa mwezi Oktoba, vipindi vya vifupi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususani katika ukanda wa ziwa Victoria, hali iliyoashiria kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli. Katika nusu ya pili ya mwezi Oktoba, vipindi vya mvua zilizoambatana upepeo mkali vilijitokeza na kusababisha uharibifu wa nyumba katika maeneo ya mikoa ya Mara, Manyara na Kigoma.

2.0 SEPTEMBA 2026

2.1 Mvua kubwa

Katika kipindi cha mwezi Septemba 2026, hali ya ukavu iliendelea kujitokeza katika maeneo mengi ya nchi. Aidha, vipindi vifupi vya mvua vilirekodiwa katika maeneo machache lakini hakuna tukio la mvua kubwa (milimita 50 kwa siku au zaidi) lililorekodiwa katika kipindi chote cha mwezi huu. Kiwango cha juu zaidi cha mvua ndani ya saa 24 kilikuwa milimita 43.6, kilichorekodiwa katika kituo cha hali ya hewa cha Pemba mnamo tarehe 18 Septemba 2026.

2.2 Hali joto

Katika kipindi cha mwezi Septemba 2026, maeneo machache sana nchini yalirekodi viwango vya joto kali vilivyofikia nyuzi joto 35°C au zaidi. Kiwango cha juu zaidi cha joto kilichorekodiwa kilikuwa nyuzi joto 36.9°C, katika kituo cha hali ya hewa cha Mpanda, mkoani Katavi, mnamo tarehe 29 Oktoba 2026.

Jedwali 1: Idadi ya siku ambazo vituo vya hali ya hewa vilirekodi viwango vya juu vya joto vilivyofikia au kuzidi nyuzi joto 35°C katika mwezi Septemba 2026.


Kanda	Kituo	Idadi ya Siku(> 35°C)	Kiwango cha Juu Zaidi kurekodiwa (°C)
Magharibi	Mpanda	8	36.9 °C

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu "N", Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

	Tabora	1	35.6 °C

Aidha, hali ya baridi ya wastani ilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi, hususani nyakati za usiku na alfajiri katika maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi na maeneo ya Kanda ya Kusini. Kiwango cha chini zaidi cha joto kilichorekodiwa katika kipindi cha mwezi huu kilikuwa nyuzi joto 7.6°C, katika kituo cha hali ya hewa cha Igeri, mkoa wa Njombe, mnamo tarehe 7 Septemba 2026.

Mwenendo wa hali ya joto la chini katika baadhi ya vituo vya hali ya hewa vilivyopo katika Nyanda za Juu Kusini Magharibi umeoneshwa hapa chini.



Kielelezo 1: Viwango vya joto la chini kwa vituo vya Uyole na Igeri katika mwezi Septemba, 2026.


2.3 Upepo Mkali

Katika kipindi cha mwezi Septemba 2026, vipindi vichache vya upepo mkali vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi, hususani maeneo ya pwani, ukanda wa kati na maeneo yanayozunguka maziwa makuu. Hata hivyo, hakukuwa na athari kubwa zilizotokana na upepo katika kipindi chote cha mwezi Septemba 2026.

3.0 OKTOBA 2026

3.1 Mvua Kubwa

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2026, vipindi vifupi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi, hususani katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hali iliyoashiria kuanza kwa msimu wa mvua za Vuli 2026, hususani katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria.
Aidha, matukio machache ya mvua kubwa yalirekodiwa katika kipindi cha mwezi huu. Kiwango cha juu zaidi cha mvua ndani ya saa 24 kilikuwa milimita 57.7, kilichorekodiwa katika kituo cha hali ya hewa cha Tanga mnamo tarehe 31 Oktoba 2026, kikifuatiwa na milimita 52.6 zilizorekodiwa katika kituo cha Mlingano siku hiyo hiyo.
Vituo vingine vilivyorekodi kiwango cha mvua cha milimita 30 au zaidi vimeoneshwa hapa chini.



Kielelezo 2: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 30 au zaidi katika mwezi Oktoba, 2026

Zaidi na takwimu zilizorekodiwa katika vituo vya hali ya hewa, taarifa zilizoripotiwa na vyombo vya habari zilionesha kutokea kwa matukio ya mvua kubwa na upepo mkali yaliyosababisha uharibifu katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Mara, Manyara na Kigoma kati ya tarehe 21 na 24 Oktoba 2026.

Katika Mkoa wa Mara, hususan Wilaya ya Bunda, mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali mnamo tarehe 21 na 22 Oktoba 2026 iliathiri Kata za Kabasa, Hunyara na Mcharo. Taarifa zilionesha kuwa zaidi ya nyumba 360 ziliharibiwa, zikiwemo nyumba zaidi ya 50 zilizobomoka kabisa.

Katika Mkoa wa Kigoma, takribani nyumba 15 katika vijiji vya Kasana na Nyarugusu, Wilaya ya Kibondo, ziliezuliwa paa kufuatia mvua kubwa na upepo mkali uliotokea tarehe 21 na 22 Oktoba 2026 (Chanzo: The Guardian).



Kielelezo 3: Nyumba iliyoharibiwa na mvua kubwa iliyoambatana na upepo mkali katika Wilaya ya Bunda, Mkoa wa Mara (Chanzo: The Respondent Online)

3.2 Hali joto

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2026, hali ya joto la wastani hadi kali ilijitokeza katika baadhi ya maeneo ya nchi. Kiwango cha juu zaidi cha joto kilikuwa nyuzi joto 36.4°C, kilichorekodiwa katika kituo cha hali ya hewa cha Mpanda, mkoani Katavi, mnamo tarehe 10 Oktoba 2026. Aidha, kituo cha Mpanda kilirekodi idadi kubwa zaidi ya siku zenye joto kali ikilinganishwa na vituo vingine, ambapo siku 20 zilikuwa na viwango vya joto vilivyofikia au kuzidi nyuzi joto 35°C.

Jedwali 2: Idadi ya siku ambazo vituo vya hali ya hewa vilirekodi viwango vya juu vya joto vilivyofikia au kuzidi nyuzi joto 35°C katika mwezi Oktoba 2026.

Kanda	Kituo	Idadi ya Siku (> 35°C)	Kiwango cha juu zaidi kurekodiwa (°C)
Magharibi	Mpanda	20	36.4 °C
	Tabora	3	35.5 °C
Nyanda za juu kaskazini mashariki	Moshi	6	36.3 °C
	Same	1	35.4 °C
	Kilimanjaro	5	35.4°C
Pwani ya Kaskazini	Dar es Salaam	1	35.2°C
	Morogoro	2	35.5°C
	Ilonga	3	35.3°C

3.3 Upepo Mkali

Katika kipindi cha mwezi Oktoba 2026, hali ya upepo wa kiwango cha chini hadi wastani ilitawala katika maeneo mengi ya nchi, huku matukio machache sana ya upepo mkali wenye kasi iliyofikia kilomita 40 kwa saa yakijitokeza katika maeneo ya pwani ya Bahari ya Hindi na maeneo yanayozunguka maziwa makuu pamoja na nchi kavu. Vipindi vya upepo mkali vilisababisha uharibifu wa mali katika maeneo yaliyoathirika.

Matukio haya ya hali mbaya ya hewa yanaonesha ongezeko la changamoto zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa na tabianchi na umuhimu wa kutekeleza mikakati thabiti ya kukabiliana mabadiliko hayo ili kulinda jamii na mazingira.

Imetolewa: tarehe 12 Novemba, 2026
Na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania.

Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania,
Kiwanja Na. 6, Kitalu “N”, Mtaa wa Fahmida, Dodoma jiji,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz